

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Idara Kuu ya Utumishi,
S. L. P. 2483,
DARES SALAAM,

Kumb. Na. EA.45/257/01

29 Agosti, 2002

Kumb. N.

**YAH. WARAKA WA UTUMISHI NA. 3 WA MWAKA 2002
UMRI WA KUSTAAFU**

Bunge ilipitisha Sheria Na. 2 ya 1999 ya Mafao ya Hitimisho la Kazi katika Utumishi wa Umma. Sheria hiyo ilianza kufanya kazi kuanzia tarehe 1 Julai, 1999. Pamoja ana Sheria hiyo bunge pia ilipitisha Sheria Na. 3 ya mwaka 1999 ya Mafao ya Hitimisho la Kazi kwa Viongozi wa Kisiasa iliyoanza kutumika tarehe 1 Novemba, 2000.

Sheria Na. 2 ya mwaka 1999 ilifuta Sheria ya Pensheni Sura 371 na inawahusu watumishi wote wa Serikali na wale wa Wakala wa Serikali (Executive Agencies).

UMRI WA KUSTAAFU KWA HIARI

Umri wa kustaafu kwa hiari umetajwa katika Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Kazi Na. 2 wa 1999 kifungu cha 17 (1) kuwa ni miaka Hamsini na tano (55). Utekelezaji wa kifungu hiki umcelezwa kuwa mtumishi atastaafu kwa hiari afikapo umri wa miaka hamsini na tano (55), na asipostaa fu wakati huo itabidi aendelee na kazi hadi atakapofikisha umri wa kustaafu kwa lazima yaani miaka sitini (60).

UMRI WA KUSTAAFU KWA HIARI KWA MAASKARI POLISI

Umri wa kustaafu kwa askari Polisi uko kama ifuatavyo hapa chini:

- (a) Police Constable and Prison Officers Grade III -miaka 45. (ii)
- (b) Corporal, Sergeants, Prisons Officer Grade I and II - miaka 50. (iii)
- (c) Askari wengine wa vyeo vya juu -miaka 60. (iv)

Kufuatana na maagizo ya Sheria hii, katika hali ya kawaada, hakuna mtumishi atakayeruhusiwa kustaafu kabla ya Julai Mosi, 2004. Katika kipindi hiki mtumishi ataruhusiwa kustaafu kutokana na sababu zilizoinishwa katika kifungu 17(3) ambazo ni;

- (a) Ugonjwa uliothibitishwa na Daktari na kuridhiwa na Mwajiri kuwa mtumishi huyo hana uwezo tena wa kufanya kazi.
- (b) Mwajiri ajiridhishe kuwa kuna umuhimu wa mtumishi huyo kustaafu.
- (c) Mwajiri inwenyewe kuona ULAZIMA wa kumwendo kazini mtumishi kwa sababu atakazozitoa.
- (d) Ikiwa ni utekelezaji wa Katiba ibara ya 72 mtumishi anaweza kustaafu.

UMRI WA KUSTAAFU KWA LAZIMA

Umri wa kustaafu kwa lazima kufuatana na Sheria niliyoitaja hapo juu utakuwa miaka sitini (60), na umri huo utakuwa kwi watumishi wote wa umma.

KUENDELEA KUFANYA KAZI NA WATUMISHI BAADA

KUTIMIZA UMRI WA KUSTAAFU

Kufuatana na sheria hii si halali kwa mtumishi aliyetimiza umri wa kustaafu kuendelea kufanya kazi bila kibali cha mamlaka husika.

Kwa muda mrefu kumekuwepo na tatizo la kuendelea kufanya kazi na watumishi amba walitakiwa wawe wamestaafu; na kisha kibali cha kuhalalisha ajira hiyo kuombwa baada ya muda kupita (Retrospective Approval). Utaratibu huo hautakuwepo, na mwajiri atakayeendelea kufanya kazi na mstaafu pasipo kufuata utaratibu itabidi awajibike. Kwa kuwa sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma inaeleza juu ya ajira ya ushindani, hapatakuwa na ajira za mkataba kwa wanaostaafu kazi, yaani kuwaombea mikataba. Ikitokea kuna kazi ambayo inatakiwa ifanywe kwa mkataba, kazi hiyo itatangazwa na kama mstaafu anazo sifa za mahitaji ya kazi hiyo anaweza kuajiriwa kama raia yeoyote wa Tanzania.

Kutokana na marekebisho haya Waraka Na. 3 wa 1971 unaufutwa na Waraka huu unaanza kutumika tarehe 1/7/1999

J. M. RUGUMYAMHETO
Katibu Mkuu (Utumishi)